https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness



https://www.path-2-happiness.com/sw

# NJIA YA ELIMU NA USTAARABU

https://www.path-2-happiness.com/sw

# Yaliyomo

**NJIA YA ELIMU NA USTAARABU**

Njia ya Elimu na Ustaarabu

Uislamu na Elimu

Njia ya Ustaarabu

Vipengele vya Njia ya Ustaarabu

Miujiza ya Qur’an na Sunnah



https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



# NJIA YA ELIMU NA USTAARABU

## UISLAMU NA ELIMU

https://www.path-2-happiness.com/sw

Hapana shaka kuwa Njia ya Furaha hapana budi kupita katika njia za elimu na ustaarabu, haiwezekani kwa hali yoyote kupita katika mabonde ya ujinga, na haipatikani dini wala fikra ambayo imenyanyua hadhi ya wanazuoni na kuheshimu miamala yao na kuhimiza kutafuta elimu na kuitumia akili na kulingania katika mazingatio na kufikiria kama mfano wa dini ya Uislamu aliokuja nao Mtume Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ambae alijenga ustaarabu mkubwa ulioenea mashariki ya ardhi na magharibi yake.

Kwa hali hiyo kutumwa kwake Swala Llahu 'alayhi wasallam kunahesabiwa kuwa ni mapinduzi ya kweli ya kielimu katika mazingira ambayo roho ya kielimu imeyazoea, Kwa hiyo Uislamu ukaja ili elimu ianze, na dunia ing'are kwa nuru ya uongofu wa Mwenyezi Mungu, Akasema Aliyetukuka: {Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya? Na nani aliye mwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini?} [5:50].

Hakuna nafasi ya ujinga kwenye dini hii au dhana au shaka, aya ya kwanza kushuka kwa Nabii Umiyyi (Swala Llahu 'alayhi wasallam): {Soma kwa jina la Mola wako Mlezi aliye umba, Amemuumba binaadamu kwa tone la damu, Soma! Na Mola wako Mlezi ni Karimu kushinda wote! Ambaye amefundisha kwa kalamu. Kamfundisha mtu aliyo kuwa hayajui.} [96:1-5].

Ikawa wazi kuwa maudhui ya kwanza ni ufunguo wa kufahamu dini hii, na ni ufunguo wa kufahamu dunia hii, bali kufahamu akhera ambayo ni marejeo ya watu wote.

https://www.path-2-happiness.com/sw



Atakayeangalia jinsi Qur-aan ilivyojali kadhia ya elimu haimdhihirikii katika mazingatio ya mwanzo kuteremshwa kwake tu, lakini ilikuwa tokea kuumbwa kwa mwanadamu mwenyewe, kama Qur-aan yenyewe ilivyolieleza hilo katika aya zake; Allah amemuumba Adam na kumfanya khalifa katika ardhi, akaamuru Malaika kumsujudia, akamkirimu na kumtukuza na kumnyanyua, kisha akatutajia sisi na Malaika sababu ya heshima, utukufu na kunyanyuliwa huku; akaainisha kuwa ni elimu Allah, Aliyetukuka amesema: {Na pale Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi), wakasema: Utaweka humo atakaye fanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutakasa kwa sifa zako na tunakutaja kwa utakatifu wako? Akasema: Hakika Mimi nayajua msiyo yajua. Na akamfundisha Adam majina ya vitu vyote, kisha akaviweka mbele ya Malaika, na akasema: Niambieni majina ya hivi ikiwa mnasema kweli. Wakasema: Subhanaka, Wewe umetakasika! Hatuna ujuzi isipokuwa kwa uliyo tufunza Wewe. Hakika Wewe ndiye Mjuzi Mwenye hikima. Akasema: Ewe Adam! Waambie majina yake. Basi alipo waambia majina yake alisema: Sikukwambieni kwamba Mimi ninajua siri za mbinguni na za duniani, na ninayajua mnayo yadhihirisha na mliyo kuwa mnayaficha?} [2:30-33].



## Soma… Huu Ndio Mwito wa Uislamu

"Hapana shaka kuwa Uislamu (ambayo ni dini ya elimu na maarifa) inawalingania wenye kuikumbatia katika kutafuta elimu na kuitumia, wala hakuna ajabu katika hilo. Kwani Ayah ya mwanzo katika Qur-aan Tukufu ni kauli yake Allah Ta'ala: "Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba."

**Robert Pierre Joseph**

Profesa wa Falsafa katika Vyuo Vikuu vya Ufaransa.

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Kinachoashiria umuhimu wa elimu na thamani yake katika Uislamu ni kuwa si tu kuwa tokea mwanzo katika Qur-aan imezungumzia masuala ya elimu katika kauli yake Allah {Soma}

bali huu ndio mfumo uliothibiti katika katiba hii ya milele, hivyo hakuna sura yoyote miongoni mwa sura zake zenye kuzungumzia elimu, iwe ni kwa njia ya moja kwa moja au isiwe ya moja kwa moja, Allah ameamrisha elimu katika jambo kubwa lenye kushuhudiwa nalo ni kumpwekesha Allah Aliyetukuka; katika kauli yake Allah Ta'ala: {Basi jua ya kwamba hapana mungu ila Mwenyezi Mungu, na omba maghufira kwa dhambi zako na za Waumini wanaume na Waumini wanawake. Na Mwenyezi Mungu anajua mahali penu pa kwenda na kurudi, na mahali penu pa kukaa.} [47:19],

Kwa hiyo ikaonyesha juu ya ukubwa wa ubora wa elimu na watu wake, imekana kulinganisha kati ya mwenye kujua na asiye jua: {…Sema: Ati watakuwa sawa wale wanao jua na wale wasio jua? Hakika wanao kumbuka ni watu wenye akili.}[39:9].

Bali Allah amewanyanyua ambao wamepewa elimu daraja la juu duniani, mbali na thawabu huko akhera. Allah amesema:{…Mwenyezi Mungu atawainua walio amini miongoni mwenu, na walio pewa ilimu daraja za juu. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.} [58:11],



## Msikiti…Chuo Kikuu

"Ndivyo misikiti ilivyokuwa hapo kabla (hata leo hii baadhi yake) imekuwa ni vyuo vikuu vya Kiislamu: Ni mshangao mkubwa kwa wanafunzi waliojawa na hamu katika elimu. Wanafunzi ambao wamekuja kusikiliza mihadhara ya wanazuoni katika elimu za dini, sheria, falsafa, tiba na hesabu. Na kwa hakika wanazuoni wenyewe wamekuja kutoka pande zote za Ulimwengu ambao walikuwa wakizungumza lugha ya Kiarabu, nao walikuwa wakimkaribisha kila mwanafunzi bila kujali utaifa wake."

**Stanley Lane-Poole**

Mwanazuoni wa Uingereza.



https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Ikutoshe kuwa haipatikani katika Qur-aan kusisitizwa juu ya kuomba ziada ya kitu chochote isipokuwa katika elimu, Allah amesema: {…Na sema: Mola wangu Mlezi! Nizidishie ilimu.} [20:114],

Wala haikuwa amri ni kwenye mlango wa kuzidisha pindi Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) aliposema: «Atakayefuata njia ya kutafuta elimu Mwenyezi Mungu atamrahisishia njia ya peponi, na kuwa Malaika wanaweka mbawa zao kwa kuridhia mtafuta elimu, na kuwa mtafuta elimu wanamuombea msamaha waliomo mbinguni na ardhini, hata nyangumi baharini, na kuwa ubora wa mwanazuoni juu ya mshika ibada (mwenye kuabudu) ni kama ubora wa mwezi kwa sayari nyinginezo, kwa hakika wanazuoni ni warithi wa Mitume, kwani Mitume hawarithiwi dinari wala dirhamu bali hurithiwa elimu, kwa hiyo atakayeichukua amechukue hadhi kubwa.» (Muslim). Na hivyo basi baada ya kutumilizwa kwake misikiti ikawa ndio kasri ya elimu na wanazuoni.

Jambo kubwa la kushtua ni pale utakapohesabu idadi ya neno "Elimu-'Ilmu" na vitoheo vyake tofauti vilivyokuja kwenye kitabu cha Allah; unapata idadi yake kufikia mara mia saba na sabini na tisa (779); kwa wastani wa mara saba kwa kila sura ya Qur-aan! Hii ni kuhusu neno elimu,

**Qur-aan na Sayansi**

"Qur-aan imekusanya ndani aya bainifu katika elimu ya mazingira (sayansi) zilizotolewa na Pro Yusuf Marwa katika kitabu chake, "Sayansi katika Qur-aan." Na ikafikia aya mia saba na sabini na nne. Na maelezo yake ni kama ifuatavyo: Hesabu aya sitini na moja, Fizikia aya mia mbili na sitini na nne, atom aya tano, Kemia aya ishirini na tisa, Vipimo vya mwendo aya sitini na mbili. Hali ya hewa aya ishirini, maji aya kumi na nne, elimu ya anga aya kumi na moja, elimu ya wanyama aya kumi na mbili, kilimo aya ishirini na moja, elimu ya viumbe hai aya thelathini na sita, Jiografia aya sabini na tatu, elimu ya nasaba za watu aya kumi, elimu ya tabaka za ardhi aya ishirini na elimu kuhusu ulimwengu na historia ya matukio yake aya thelathini na sita."



**Maurice Buccaile**

Mwanazuoni na tabibu wa Kifaransa.

hata hivyo kuna maneno mengi yenye kuashiria maana ya elimu lakini hayakutajwa kwa tamko lenyewe; mfano: Yakini, uongofu, akili, kufikiri, kuangalia, hekima, fiqhi (kujua), Burhani, dalili, hoja, aya (alama) ubainifu na mengineyo yasiyokuwa hayo katika maana yanayotokana na elimu na kuhimiza elimu yenyewe, ama sunnah ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kuhesabu neno hili ni vigumu kwa wingi wa ilivyoelezwa.

Qur-aan sio kitabu cha Physics, Chemistry, Biology au hesabu, bali ni kitabu cha Uongofu pamoja na hayo haukusaza chochote kulichothibitishwa na sayansi ya kisasa.

Hayo yalikuwa na athari kubwa katika dola ya Kiislamu baada ya hapo; kwani kulikuwepo na harakati kubwa kabisa za kielimu katika nyanja zote za elimu na mataifa, harakati na nguvu ambazo hazijawahi kuwepo mfano wake katika historia; jambo ambalo lilifanya ustaarabu na maendeleo makubwa kufikiwa katika mikono ya wanazuoni wa Kiislamu, na kumpa urithi binadamu kwa silaha nzuri za elimu ambayo dunia nzima inadaiwa na Uislamu.

MarxMarhaaf anasema: "Maendeleo ya Chemistry Ulaya yanarejewa kwa Jabir bin Hayyan moja kwa moja, na dalili kubwa ya hilo ni kuwa Istilahi nyingi alizozigundua bado hutumika katika lugha mbali mbali za Ulaya."

Ama Aldo Mieli anasema: "Na tukihamia katika elimu ya sayari (astronomy), tokea mwanzo tutawaona wanazuoni wa sampuli ya kwanza, na miongoni mwa wanazuoni hao maarufu ni Abu Abdullah Muhammad bin Musa Al-Khawarizmy.(Mwanzilishi wa elimu ya Aljebra na kujua mfumo wa idadi ya kihindi na ameweka misingi ya tafiti za hesabu, elimu za unajimu (astronomy) na Jiografia.)

Al- Khawarizmy alikuwa ndie mfunguzi wa mnyororo wa wanazuoni wakubwa wa mahesabu, na vitabu vyake viliendelea kusomeshwa katika vyuo vikuu vya Ulaya hadi karne ya kumi na sita."

Zaghrid Honka amesema katika juzuu maalumu kuhusu operesheni katika kitabu: "Ubainifu kwa aliyeshindwa kutunga." Cha mwandishi: Az-Zahrawy; (Ni kitabu kinachokusanya maarifa yote ya tiba katika mijaladi thelathini. Kina picha mbali mbali, na maumbo ya vyombo na vifaa alivyokuwa akitumia mwandishi wake Az-Zahrawiy katika operesheni zake, kimefasiriwa na Gerald Al-Karmuni juzuu maalumu inayohusiana na mas-ala ya operesheni katika kitabu hiki kwa lugha ya kilatini katika karne ya kumi na mbili Miladiy. Chapa mbali mbali zilishatoka hapo zamani, ya kwanza huko Bundukia (Venice) mwaka 1497 AD. Na ya pili ni huko Bazli mwaka 1541 AD na ya tatu Oxford mwaka 1778 AD kama ambavyo Dr. Lucklirk alifasiri katika lugha ya kifaransa katika karne ya kumi na tisa.) (sehemu ya tatu ya kitabu hiki kimekuwa na nafasi muhimu sana Ulaya ambapo paliwekwa misingi ya operesheni Ulaya, tawi hili la tiba likawa lipo kileleni, hivyo masuala ya opereshenіyakawa yanajitegemea katika misingi yake katika elimu za upasuaji."

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Kitabu cha Az-Zahrawy kilikuwa na athari kubwa katika kuinyanyua Ulaya kwa muda wa karne tano, ambapo kilikuwa kikifundishiwa katika vyuo vikuu vya Ulaya, kama ambavyo wapasuaji wengi wa Ulaya wakidondoa humo na kuchukua.

Bado wanazuoni wa Kiislamu waliendelea kutoa michango yao kwa wanadamu wote; Ahmad Zuwayl (Huyu ni mwanakemia wa Kimisri, aliwahi kupata zawadi ya Nobel mwaka 1999AD kwa ugunduzi wake wa Camera ya kuchambua spectra (mpangilio maalum wa taswira zinazotokana na miali ya mnunurisho), Kamera ambayo inafanya kazi kwa spidi ya Femtosecond (Femtosecond Spectroscopy). Na utafiti wake kuhusu maingiliano na kikemia kwa matumizi yake. Hii imesaidia ulimwengu kuingia katika mas-ala ambayo mwanadamu hakuweza kutaraji kuyafahamu, ili kuweza kuona na kufahamu harakati za vitu vidogo sana wakati wa muingiliano wa kikemia kwa njia ya Teknolojia ya Laser kwa njia ya haraka zaidi. Dr. Ahmad Zewail aligundua mfumo wa upigaji picha wa haraka zaidi inatumika kwa njia ya laser, yenye uwezo wa kufuatilia harakati za protons wakati wa kukua kwake na wakati wa kukutana pamoja, na unit ya muda ambayo picha inapiga ni hiyo Femtosecond, nayo ni sehemu ya Bilioni ya sehemu ya sekunde. ) anasema: katika kitabu chake, Zama za Elimu: (kazi yangu kubwa ilikuwa ikiangukia kwenye sehemu maalum



**Mapenzi ya kuelimika.**

"Haikuwahi kutokea katika Historia ya maendeleo Ulimwenguni harakati yenye kufurahisha kuliko mapenzi ya ghafla ya utamaduni. Kama ilivyotokea katika sehemu zote za ulimwengu wa Kiislamu: Ikawa kila Muislamu kwa khalifa kuwa ni msanii (mtengenezaji) kama kwamba ghafla tu amekumbwa na shauku ya elimu na kiu ya safari (kutafuta elimu). Haya yakawa ni mambo ya kheri Uislamu ulioyaleta kutoka pande zote. Wanafunzi walisongamana katika vituo kama vile Baghdad. Na baada ya hapo katika vituo vingine ambavyo vilikuwa ni mbeleko ya adabu na elimu, mfano wake ni harakati mpya za wanazuoni wa ulaya ambao walifurika katika vyuo vikuu kuchukua elimu mpya. Bali kwa hakika lilikuwa ni jambo zuri."

**Stanley Lane-Poole**

Mustashrik wa Uingereza.

katika moyo wa atoms, ambapo kuna kukutana na kuna kuachana kwa vitu katika milango ya fahamu, kama ambavyo muda ulivyo ndani ya sekunde; ambapo sekunde huwa ni muda mkubwa."

Wala hakuna ubishi kuwa elimu hii, uongofu, na nuru aliyokuja nayo Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) imemtoa mwanadamu kutoka katika makutano ya maji ya Asina (yaliyobadilika rangi), hivyo akainyanyua kwa elimu, ustaarabu na utamaduni kwa muda wote wa historia.

Uislamu ukaja kwa mfumo wa kielimu na kisayansi, kwa mfano Uislamu unahadharisha kuiga kibubusa bila kutumia akili; anasema Subhaanahu kuhusu washirikina: {…wao husema: Bali tutafuata tuliyo wakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawaelewi kitu, wala hawakuongoka?} [2:170],

Na kufuata dhana bila kufuata mfumo wa kielimu; Allah Aliyetukuka amesema: {… Hawa hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kusema uwongo tu.} [6:116]

Na kuhusu matamanio ambayo yanakwenda kinyume na elimu, mantiki, akili na utafiti; Allah amesema: {…Na hakika wengi wanapoteza kwa matamanio yao bila ya kuwa na ilimu….} [6:119],

Na kuhusu bughudha na chuki ambayo inamuweka mtu mbali na uadilifu amesema: {…Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.} [5:8],



## Ustaarabu wa Elimu

"Kila tunapoangalia kwa kina ustaarabu wa Waarabu, vitabu vyao vya kielimu. Uvumbuzi wao, fani zao, inadhihiri kwetu ukweli mpya na upeo mpana. Na kwa haraka tumewaona Waarabu kuwa ndio watu bora katika karne za kati (Middle age) kuwa na maarifa kwa ajili ya elimu za waliotangulia.
Kwa muda wa karne tano vyuo vikuu vya Magharibi (Ulaya) vilitegemea vyanzo vya elimu na machapisho ya Waarabu. Nao ndio ambao waliiendeleza Ulaya kwa akili na tabia njema. Historia haijawahi kufahamu Ummah uliozalisha kama walivyozalisha Waarabu (Waislamu) kwa muda mfupi na hakuna watu wengine waliowafikia katika uvumbuzi na fani zingine."

**Gustaf Lubon**

Mwanahistoria wa Ufaransa.

https://www.path-2-happiness.com/sw



**Qur-aan ni Miujiza**

"Kwa hakika nimefuatilia aya zote za Qur-aan ambazo zina uhusiano na sayansi na mazingira nikazikuta kwamba aya hizi zinakubaliana na elimu zetu mpya.
Nimeyakinisha kuwa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi Wasallam) amekuja na ukweli ulio wazi kabla ya miaka elfu moja, na kabla ya kuwepo mwalimu yoyote miongoni mwa wanadamu. Lau kila mwenye elimu au fani angelinganisha vizuri aya zote za Qur-aan zinazohusiana na alichokisoma, kama nilivyolinganisha bila shaka angetii Qur-aan, ikiwa ana akili ameepukana na hisia za chuki."

**Rene Guenon**

Mwanafalsafa wa Kifaransa

https://www.path-2-happiness.com/sw

Na kuhusu uwazi wa usio na upendeleo kuhusu elimu; Allah Ta'ala amesema kuhusu Mayahudi: {Miongoni mwa Mayahudi wamo ambao hubadilisha maneno kuyatoa mahala pake, na husema: Tumesikia na tumeasi…} [4:46]

Na kuhusu kutofanya dhuluma na uharibifu amesema Aliyetukuka: {Bali lawama ipo kwa wale wanao wadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika nchi bila ya haki. Hao watapata adhabu iliyo chungu.} [42:42]

Na kuhusu amana ya kielimu pamoja na uadilifu baina ya watu; amesema: {…Na mnapo hukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu….} [4:58],


Na uadilifu, unyoofu na kushuhudia haki; Amesema: {Enyi mlio amini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapo kuwa ni juu ya nafsi zenu…} [4:135],

Ama kuhusu umuhimu wa utafiti wa dalili na hoja amesema: {Sema Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli.} [27:64]:

Na mengi yasiyokuwa hayo yenye kujenga na kutengeneza mfumo wa kisomi kwa njia ya sayansi na ustaarabu.



https://www.path-2-happiness.com/sw



## Mfumo Bora

"Uislamu ulifanikiwa: Kwa sababu ulikuwa ni mfumo bora wa Kijamii na kisiasa ambao siku ziliweza kuutanguliza (mbele). Nao ulisambaa. Kwa sababu kila ulipokwenda ulikumbana na mataifa yaliyokuwa nyuma kisiasa. Mataifa ambayo yalikuwa yakinyang'anya raia zake, yakidhulumu na yakiwahofisha wala hayakusoma wala kuwa na utaratibu wowote, vile vile ulikuta serikali hizo zina ubinafsi na ugonjwa hazina uhusiano baina yake na watu wake. Hivyo Uislamu ukabaki ndio fikra safi zaidi ya kisiasa na utendaji mzuri ulimwenguni hadi muda ule ulikuwa ukiwatumikia watu kwa mfumo bora kuliko nidhamu yoyote nyingine. Ama mfumo wa Kibepari ulikuwa ukiwafanya watu kuwa ni watumwa katika ufalme wa Roma. Elimu, fasihi na taratibu na ada na kijamii huko Ulaya zilikwisha anguka kabla ya Uislamu kuibuka."

**H. G. Wells**
Mwandishi

# NJIA YA USTAARABU

Hakuna umma, kundi, taifa iwe ni la kijima au la kisasa, ambalo litakuwa na utamaduni ambao unawaunganisha na kuwapa tabia pambanuzi, utamaduni ni njia katika kuishi, ni sehemu ya maisha na uwepo, ni mfumo wa maadili na kijamii ambayo yanahukumu mandhari ya maisha na vipengele vyake vyote, hili linaakisiwa katika mambo ya nguvu na tabia zote na kuipa jamii kitambulisho chake na kuhifadhi mshikamano wake.

Ama ustaarabu huu ni wasifu wa ziada wa uwepo kwa utamaduni wa kijamii ambao unabeba maana ya maendeleo, na kupanda (kuendelea) kwa pande zote mbili ya aina na idadi, na hivyo kupata mafanikio katika uhalisia wa mambo, ni hatua inayoonekana katika athari ya mazingira katika historia yenye uwezo wa kutengeneza matukio yake na kuyaelekeza, harakati zinaweza kufikia kiasi cha kutengeneza bonde linatotenganisha zama na mahali.

Na hivi ndivyo ambavyo ustaarabu unavyowakilisha hakuna mfano wake katika tabia na mazingira, siasa na dini, utamaduni na sayansi na Akhlaqi, vipengele vyote hivi tunaviona vikitoka katika chombo kimoja nacho ni ustaarabu wa watu hawa au wale kwa tabia zao za kipekee.

Uislamu umefanikiwa kubadilisha nafsi za kundi la mwanzo lililoamini kutoka katika maisha ya kibedui ambayo ilikuwa yakitawaliwa na kasumba na kuwa nyuma na kuwafanya kupambika kwa tabia tukufu na kwa muda mfupi maendeleo na ustaarabu ukasambaa duniani na watu wengi wakaitikia kwenye ustaarabu huu wakati ule kwa wepesi wa dini aliyobashiriwa nayo Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam), uadilifu, udugu na usawa, ustaarabu huu ulikuja wakati ambapo binadamu alikuwa amekwisha choshwa na mfumo wa zamani uliosimamishwa kutokana na

https://www.path-2-happiness.com/sw


https://www.path-2-happiness.com/sw

utumwa na udikteta, kwa hiyo wakaukumbatia mfumo mpya ambao ndani yake waliona utukufu na utu wao baada ya kuonja dhulma na ukandamizaji chini ya wafalme, makuhani na utawala wa kidikteta wa mtu mmoja.

Kwa hiyo Uislamu ukawa ndio fursa yao ya dhahabu, kwani Uislamu huo ulitengeneza mambo yao mengi na ndani yake wakaona maisha matukufu ambayo walikuwa wakiyatamani, na wakati huo huo ikawaondoshea dhuluma, ujinga na ujima.

Ustaarabu wa Kiislamu umeheshimu mtazamo wa binadamu; haukuwahi kumtofautisha hata siku moja kati ya mtu na nduguye, kwa misingi ya ubaguzi wa rangi au lugha, bali umewapa wote muamala mmoja na haki sawa kwa wote, na hivyo Ustaarabu ukachangia maendeleo ya wanadamu baada ya kubadilisha mfumo wa kikabila ambao unasimama katika uhusiano wa damu na nasaba kuelekea katika mfumo wa kundi unaoshirikiana katika itikadi na fikra ambayo inasimama katika mashirikiano ya kijamii kwa misingi ya udugu na usawa.

Lengo la kwanza la Ustaarabu kwa mtazamo wa Uislamu ni kufanikisha utulivu, usalama na amani na kusimamisha jamii bora na kuwafurahisha wanadamu katika yaliyokuwa ya kheri, kadhalika kupiga vita matendo yote ya shari; ambapo maendeleo yote, ustaarabu na tamaduni zote lengo lake sio ustaarabu wenyewe kwani malengo halisi ya ustaarabu sahihi ni kufikia katika furaha ndani ya nafsi ya mwanadamu na utulivu katika moyo wake na kwenda pamoja katika kufikia amani na maendeleo ya jamii pamoja na mataifa, na



**Miongoni mwa Alama za Kughurika.**

"Hakika ni wakati muafaka kufanya utafiti kuhusu athari za Kiislamu juu ya Ulaya kwa wakati huu ambapo uhusiano kati ya Waislamu na Wakristo Waarabu pamoja na Wazungu wa Ulaya unaongezeka katika ulimwengu huu mmoja. Kwani imewahi kuonekana wakati fulani kabla katika karne za kati waandishi Wakristo wa Ulaya walitengeneza sura chafu kuhusu Uislamu katika maeneo mengi: Hata hivyo kwa fadhila za jaribio la watafiti katika karne iliyopita sura sahihi zaidi ya kuangalia mambo kwa mtazamo usio na upendeleo imeanza kutengenezwa katika akili za watu wa Magharibi: Na kwa sababu ya kuwepo mahusiano mzuri na Waarabu na Waislamu basi ni juu yetu kutambua fadhila zote tulizofanyiwa na Waislamu. Ama jaribio letu la kukana hayo ni alama miongoni mwa alama za uongo za kudanganyika."

**W. Montgomery Watt**

Mustashrik wa Uingereza.

hilo kupitia kufikia katika yaliyokuwa ya kheri na yenye manufaa na kuwa mbali na kila yaliyokuwa ya shari na yenye kudhuru

ambayo ni kinyume na ustaarabu wa kisasa ambayo umemuongezea mwanadamu khofu na wasi wasi na kumswaga mwanadamu katika upotofu wa kimaada unaoangamiza na kuwa mbali na tabia njema, fadhila na dini na mfano wake katika thamani za utu wa mwanadamu, hali ambayo (kwa ustaarabu mambo leo) umemfanya mwadamu kuwa ni chombo (mashine) kisichokuwa na roho ambayo mwenye nguvu humsaga mnyonge.



**Kuanguka kwa Ulimwengu.**

"Magharibi kwa sasa wana haja ya Uislamu kuliko muda wowote uliopita ili kuyapa maisha maana na historia makusudio yake, hadi Wamagharibi waweze kubadili tabia yao ya kutenganisha kati ya elimu na imani. Uislamu hauweki kizuizi kati ya elimu na imani, bali kinyume chake unaunganisha baina yake kwa kuzingatia kuwa hicho ni kitu kimoja kisichowezakugawanyika. Kama ambavyo inawezekana kwa Uislamu kurejesha uhai wa matarajio ya jamii yetu mpya iliyoathirika na upweke (ubinafsi) wa njia ambayo inaupeleka ulimwengu kwa ujumla wake kuanguka."

**Marmaduke Picthall**

Mwanafasihi na Mwanafikra Mwingereza



**Mafanikio ya Kielimu**

"Uislamu umepata mafanikio makubwa ya kielimu zaidi ya karne nane: Hivyo basi ni makosa kudhania kuwa Uislamu ni kunakili Ustaarabu tu. Au kuwa ustaarabu mpya ni wa Magharibi kwa vile umekamilika. Uislamu una fadhila kubwa katika kuweka kanuni za awali ambazo zimepelekea mafanikio hayo."

**Prince Charles**

Mwanamfalme wa Uingereza

## VILINZI VYA NJIA YA FURAHA

Ustaarabu wa Kiislamu una vidhibiti bainifu na wasifu uliokuwa wazi ambao unatengeneza haiba ya mtu mkamilifu vidhibiti vyenye alama zenye kujitegemea na nyinginezo kwa misingi ya ustaarabu, malengo yake na misingi yake pamoja na kuwepo kiasi cha ushirikiano kati yake na tamaduni nyingine.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Misingi ya ustaarabu wa Kiislamu sio tu kutukuza akili kama ilivyokuwa kwa Wagiriki, wala kutukuza nguvu na utawala kama ilivyokuwa kwa Waroma, au kuupa umuhimu matamanio ya kiwiliwili na nguvu za kijeshi na siasa kama ilivyokuwa kwa wafursi au kujenga nguvu za kiroho kama walivyofanya Wahindu na baadhi ya Wachina au nguvu na utawala wa 'watu wa dini' pamoja na upotofu ambao ulipelekea kwenye kiza katika karne ya kati huko Ulaya.

Kadhalika sio kama ilivyo hivi sasa ambapo fitna ya sayansi na elimu na maada na kiasi binadamu kufaidika na silaha na hazina zilizokuwepo ulimwenguni kwa maada yenye kuangamiza kama tunavyoona leo hii katika mfumo wa ustaarabu huu uliorithiwa kutoka kwa Wagiriki na Warumi.

Ama misingi ya Ustaarabu wa Kiislamu una Tawhidi, kufikiri, elimu, matendo, roho, kujenga, kuheshimu akili na kuheshimu mwanadamu, yaani kwa vile inavyokusanya sehemu zote za maisha ya mwanadamu, na hili ndilo lililofanya Ustaarabu huu wa Kiislamu uwe unajitegemea kwa ukamilifu yenye desturi pana maalumu inatofautiana kwa tofauti kubwa na misingi ya staarabu nyinginezo.

Ustaarabu wa Kiislamu upo juu ya staarabu nyingine kwa kuwa na nguvu ya kiroho, kijihadi, kujitahidi, usawa, uadilifu, msamaha pamoja na wenye kutofautiana nao, na kadhalika kupenda kheri na kueneza sayansi ulimwenguni kote, na kwa hilo basi ustaarabu huu unapendekezwa kwa mara nyingine tena kuwaongoza wanadamu kwa hoja ya kumiliki vidhibiti hivi.

**Karne ya Kati**

"Lau Musa bin Nasir angewafikisha kuichangua Ulaya; Basi angeifanya Ulaya nzima kuwa ni ya Kiislamu, na angeiokoa Ulaya (bila ya shaka) katika duru ya karne ya Kati ambayo Uhispania haikuweza kujua na kusimama ila kwa fadhila za Waarabu."

**Gustaf Lubon**
Mwanahistoria wa Kifaransa




## Uislamu unajipambanua kwa vipambanuzi vingi katika hivyo ni:

### 1. Imani na Tawhidi:

Imani inahesabiwa kuwa ni kiini cha njia ya furaha na linganio kubwa kwenye kutafuta elimu na kujenga ustaarabu, na kila ustaarabu ambao hautosimama katika imani ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) na tawhidi yake ni ustaarabu wenye mgogoro ndani yake, wenye kupigana vita kati ya sehemu

https://www.path-2-happiness.com/sw



**Arnold J. Toynbee**

Mwanahistoria Mwingereza.

## Ushindi wa Mateka.

“Uislamu uliziteka nchi zilizoishinda katika vita vya msalaba na hivyo kuingiza fani mbali mbali na ustaarabu katika maisha ya ulimwengu wa Wakristo. Maisha ya walatini yalikuwa na kutu katika baadhi ya makonde ya harakati ya mwanadamu, kwa mfano kama vile uhandisi wa ujenzi. Athari za Uislamu ziliingia katika ulimwengu wa Kikristo muda wote wa karne ya kati. Ama Sicily na Andalusia (Hispania) athari ya ufalme mpya wa Waarabu ulidhihirika zaidi na kupanuka.”

zake, baadhi yake kuangamiza zingine, ambapo huwafanya asiyekuwa Allah kwa miungu mingine kwa kutofautiana majina, ambayo hupelekea kwenye ufisadi wa maisha ya mwanadamu na uovu wake!! Allah amesema: {Lau wangeli kuwamo humo miungu wengine isipo kuwa Mwenyezi Mungu basi bila ya shaka hizo mbingu na ardhi zingeli fisidika. Subahana ‘Llah Ametakasika Mwenyezi Mungu, Bwana wa A’rshi (Kiti cha Enzi), na hayo wanayo yazua.} [21:22],

Na akasema Aliyetukuka: {Mwenyezi Mungu hana mwana yeyote, wala hanaye mungu mwengine. Inge kuwa hivyo basi kila mungu angeli chukua alivyo umba, na baadhi yao wangeli washinda wengine. Mwenyezi Mungu ameepukana na sifa wanazo msifu.} [23:91]

Na Akasema tena Aliyetukuka, {Sema: Lau kuwa wangeli kuwa pamoja naye miungu mingine kama wasemavyo, basi wangeli tafuta njia ya kumfikia Mwenye Kiti cha Enzi.} [17:42]

Na kinachoakisi haya ni kile kilichotokea na kinachoendelea kutokea sana katika tamaduni nyingine, na hivyo kupoteza malengo yake, na kupotoka kilichoelekezwa kwake; na hivyo kumpa mwanadamu uovu hata kama ilikusudia kumpa kheri, Allah amesema: {Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu, na pia Masihi bin Maryamu. Na wala hawakuamrishwa isipo kuwa wamuabudu Mungu Mmoja, hapana mungu ila Yeye. Subhanahu, Ametakasika na hayo wanayo mshirikisha nayo} [9:31].



**K. Lal Gaba**

Mwanasiasa na Mwanahabari wa India.

## Unaingia katika Maisha

“Uislam ndio dini bora kwa mwanadamu: Uislamu ndio ambao unaingia ndani ya maisha ya Muislamu katika vipengele vyake vyote, bali ndio kipambanuzi cha mwisho katika kila shughuli anayofanya Muislamu. Hakuna dini nyingine zaidi ya Uislamu ambayo ina uwezo wa kutatua matatizo yote ya watu katika Ulimwengu huu leo hii. Na huu ndio ubora pekee wa Uislamu.”

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

## 2. Sifa ya Kilimwengu:

Uislamu ni dini ya ulimwengu, imekuja iwe ni kwa zama na mahali pote na kwa kila lugha na watu wote, kwa kila rangi na taifa, Allah Aliyetukuka amesema:{Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji. Lakini watu wengi hawajui.} [34:28],


Na Allah akasema: {Ametukuka aliye teremsha Furqani kwa mja wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote.} [25:1],

Na akasema tena: {Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote, niliye tumwa na Mwenyezi Mungu Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi….} [7:158]

Na akasema tena Aliyetukuka, {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.} [21:107].

Hivyo basi Uislamu ukaja na itikadi thabiti ambayo haibadiliki kwa kubadilika hali, na sheria iliyosimama kwa misingi ya uadilifu, haki na kheri inayowiana na tabia ya mwanadamu katika kila zama na mahali na sababu yake ni kuwa inatoka kwa Allah ambae hufahamu yenye kufaa viumbe vyake, Allah amesema: {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari? } [67:14],

Kama ambavyo Uislamu sio dini mahususi kwa kundi au rangi au taifa maalumu la watu, Uislamu ni kwa ajili ya weupe, weusi, watu wa manjano, wekundu, nayo ni kwa ajili ya zama zilizopita na zama zilizopo na zama zijazo, wala mtafiti vyovyote atakavyopewa uwezo mkubwa wa kielimu hataona aliyokuja nayo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) hisia yoyote ya kimajimbo, au ya kikundi



**Yuko wapi Kiongozi Afaae?**

"Akipatikana kiongozi anayefaa ambaye atazungumza maneno yanayofaa kuhusu Uislamu. Basi kuna uwezekano wa dini hii kuibuka tena kama ni moja ya nguvu kubwa za msingi za kisiasa ulimwenguni kwa mara nyingine."

**W. Montgomery Watt**

Mustashrik wa Uingereza.



https://www.path-2-happiness.com/sw


au kitabaka, na hiyo ni alama ya wazi kuwa Da’wah yake ni ya Kilimwengu haitegemei kwa kundi maalumu au taifa maalumu; kwani ibada za Kiislamu, sheria zake, hukumu zake, tabia zake zote zinafaa kwa watu wote katika zama zote;

hivyo basi haiwezekani kusema kuwa uadilifu au tabia njema haifai watu fulani au zama fulani, na hili ni maalumu kwa Uislamu.

Ama katika baadhi ya dini zile hisia za kimajimbo au za kitaifa au za kujuana zipo wazi sana; kwa mfano Mayahudi wanapoamiliana na wasio katika dini yao Mwenyezi Mungu anawaelezea: {Na miongoni mwa Watu wa Kitabu yupo ambaye ukimpa amana ya mrundi wa mali atakurudishia, na miongoni mwao yupo ambaye ukimpa amana ya dinari moja hakurudishii isipo kuwa ukimsimamia kumdai. Haya ni kwa kuwa wakisema: Hatuna lawama kwa ajili ya hawa wasio jua kusoma. Na wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu, hali nao wanajua.} [3:75].

**Injili ya Mathayo**

“Akajibu, akasema, “Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea katika nyumba ya Israeli.”
Na alipowachaguwa watu kumi na wawili ili wakawalinganie mayahudi aliwausia: “Hao Yesu aliwatuma, akawaagiza, akisema, katika njia ya mataifa msiende, wala katika mji wowote wa Wasamaria msiingie. Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. Na katika kuenda kwenu, hubirini mkisema, Ufalme wa mbingu umekaribia.”





2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw




www.path-2-happiness.com/sw

## 3. Ustaaabu wa Elimu, Kuimarisha na Kujenga:

Mtazamo wa Uislamu kwa mwanadamu ni kuwa Allah amemuumba kwa ajili ya Ukhalifa na kuimarisha Ulimwengu, Allah amesema: {…Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo….} [11:61],

Na akasema Aliyetukuka: {Yeye ndiye aliye kufanyeni manaibu katika ardhi. Na anaye kufuru, basi kufuru yake ni juu yake; na kufuru za makafiri haziwazidishii kwa Mola wao Mlezi ila kuchukiwa. Wala kufuru za makafiri haziwazidishii ila khasara.} [35:39],



### Kujenga na Kuimarisha

"Uislamu unatambua kuimarisha vipaji; uzamifu na upembuzi binafsi: ni dini ya kujenga na kuimarisha na sio dini ya kubomoa. Kama kwa mfano mtu anamiliki ardhi na yeye kwa upande mwingine ana utajiri ambao hataki kulima ardhi ile na akaiacha tupu, baada ya muda fulani ardhi ile itahamia katika ardhi za Ummah katika hali ya kawaida. Sheria ya Kiislamu inathibitisha kuwa miliki ya ardhi hiyo itahamia katika mkono wa mtu wa kwanza ambae atalima ardhi ile."

**Sir Charles Edward Archibald.**

Mwanasiasa wa Uingereza.



### Kunyoosha Nafsi

"Uislamu ni dini ambayo ina afikiana na ugunduzi wa elimu, na kubwa katika hayo ni kuzinyoosha kuzipeleka kwenye Uadilifu, wema na kusameheana."

**Gustof Lubon**
Mwanahistoria Mfaransa.

Hivyo ndani ya dini ya Kiislamu watu hupata dhambi watakapoacha elimu yoyote inayomfaidisha mwanadamu na kuimarisha ulimwengu, wakati ambapo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ametumwa wakati watu wakiishi katika shimo la ujima wa ustaarabu na elimu, na watu kushughulishwa na falsafa, majadiliano kinyume na kujenga, kutenda na kuimarisha ardhi; hivyo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akawanyanyua wanadamu kwa dini ya Uislamu, dini ya Ustaarabu na dini ya kujenga bila ya kuwepo mgongano kati yake na kuimarisha ardhi, na kati yake na kunawirisha roho, hivyo hamna migongano ndani ya nafsi ya Muislamu baina ya ibada na matendo, na kuimarisha ardhi na kati yake na maisha ya kiroho na kutenda katika kumridhisha Mola wake, yote hayo ni kwa ajili ya Allah na katika njia yake, Allah Aliyetukuka amesema: {Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.} [6:162].



www.path-2-happiness.com/sw



**Juu ya Vichwa vya Mashahidi.**

"Nyote mnafahamu kuwa mimi ni "Heral" mtoto wa kiongozi mkubwa wa Kipagani, "Ghandi". Mimi natangaza mbele ya vichwa vya mashahidi na katikati ya kundi kubwa hili la Waislamu kuwa mimi nimeupenda Uislamu, nimeipenda Qur-aan na nimemuamini Allah Peke Yake na Mtume wake mtukufu Sayidina Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kuwa yeye ni Mtume wa mwisho na kuwa hakuna nabii baada yake na Qur-aan ilichokileta ni haki na vitabu vyote viliyoteremshwa ni haki. Mitume na manabii wote ni haki. Na kwa Uislamu na Qur-aan nitaishi na kufa kwa ajili yake na nitautetea na kupigana kwa ajili yake na nitakuwa moja ya nguzo yake imara na nitaulingania kati ya jamaa na ndugu zangu. Dini hii tukufu ni dini ya elimu, utamaduni, uadilifu, uaminifu, rehema na usawa."

**Abdullah Harlal Ghandi,**
Mtoto wa Mahatma Ghandi

## 4. Ustaarabu wa Kimaadili:

Tabia njema katika Uislamu ni ibada, bali Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ametujulisha kuwa lengo la kutumwa kwake ni kukamilisha Matukufu ya maadili; amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): «Nimetumwa kukamilisha matukufu ya tabia.» (Imepokewa na Malik), hivyo basi njia ya ustaarabu na furaha ni njia ya kimaadili inahimiza matukufu ya tabia na matendo mema, na maadili katika Uislamu ni mpana katika nyanya zote za maisha, mfano wa mtu kuamiliana na nafsi yake pamoja na Allah na wengine, kama inavyokusanya muamala wa Muislamu pamoja na kafiri na pamoja na mdogo na mkubwa na mwanamume na mwanamke na mtu na mtesi wake.


Hivyo basi Uislamu ukaamrisha ukarimu, ushujaa, na uadilifu, rehema na huruma, kutojikweza, adabu njema katika miamala na watu, ukweli, haya, uvumilivu, amani ya moyo na kupenda kheri na yasiyokuwa hayo, Allah Aliyetukuka ameelezea umuhimu na wajibu wa kufanya uadilifu hata ikiwa ni mtu na mtesi wake: {Enyi mlio amini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.} [5:8],

Na akasema kuhusu ujumbe wa Mtume Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kubainisha kuwa yeye ni rehema kwa walimwengu wote na sio mahsusi kwa waliomuamini peke yake tu, Allah aliyetukuka

https://www.path-2-happiness.com/sw



https://www.path-2-happiness.com/sw



amesema: {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.} [21:107],

Tabia hizi ni sehemu muhimu katika ustaarabu wa Kiislamu na nguzo yake ya asili, ndani yake, wala haiwezekani kupotea tabia njema kwa Muislamu kwa sababu yoyote ile kwa ajili ya kujenga ulimwengu huu au kwa ajili ya maslahi yoyote au yasiokuwa hayo, Allah amemtengeneza Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kumpa adabu ili awe mfano katika adabu na maadili na kigezo chema katika kila kitu, Allah amesema: {Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana} [33:21],

Na Allah akaelezea sehemu ya rehema yake na pupa yake katika kuwaongoza watu kwenye uongofu katika njia ya furaha, Allah Aliyetukuka amesema: {Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.} [9:128].

https://www.path-2-happiness.com/sw



https://www.path-2-happiness.com/sw

## 5. Ustaarabu wa Akili na Kufikiri:

Katika dini ya Uislamu hakuna ukahanuti (siri zinazotawaliwa na makuhani na watu wa dini) ambao huwezi kuuliza au siri ambayo hauwezi kuzingatia, bali Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) ameamrisha kufikiria katika aya zake, katika viumbe na katika Ummah mbali mbali, Allah Aliyetukuka amesema: {Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.} [3:191],

Na Allah Aliyetukuka akasema tena: {…Namna hivi tunazipambanua Ishara zetu kwa watu wanao fikiri.} [10:24],

Na Allah Aliyetukuka akasema: {Kwa Ishara wazi na Vitabu. Nasi tumekuteremshia wewe Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyo teremshwa kwao, wapate kufikiri.} [16:44],

Na akasema Aliyetukuka: { Je! Hawajifikirii nafsi zao? Mwenyezi Mungu hakuumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yake ila kwa Haki na kwa muda maalumu. Na hakika watu wengi bila ya shaka ni wenye kukataa kuwa watakutana na Mola wao Mlezi.} [30:8]

Na akasema tena Aliyetukuka, {…Na hiyo mifano tunawapigia watu ili wafikiri.} [59:21],

Bali Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) ametufundisha kuwa elimu sio dhana peke yake bali hapana budi elimu hiyo iwe na dalili inayosimamia, Allah Aliyetukuka amesema: {…Sema: Leteni ushahidi wenu kama nyinyi ni wasema kweli} [2:111]

Hivyo hakuna siri anayoifahamu mtu au kuhani au kiongozi wa dini ambaye hatoi siri hiyo kwa mtu.

## 6. Ustaarabu wa Amani ya Ndani na Nje:

Amani ya ndani ina maanisha furaha ya ndani ya mwanadamu na kuokoka kwake na migongano ya ndani ambayo huwakumba watu wengi katika ustaarabu wa kisasa; kiasi cha kuwa dunia na akhera zikaishi katika fikra ya amani ya mwanadamu na hivyo ibada na matendo na ujenzi wa ardhi kuishi pamoja, roho na mada, elimu na dini, hakika amani ya ndani katika ustaarabu wa Uislamu ni alama ya wazi inayotokana na tawhidi ambayo inakusanya yote yaliyotangulia katika nafsi ya muumini kwa wepesi na urahisi.

Katika Uislamu dunia si lengo katika dhati yake, bali ni shamba la akhera, mapito na kivuko cha kuelekea huko, na hili lipo wazi katika kauli yake Allah Aliyetukuka:

{Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi.} [28:77];

Na, {Na itakapo kwisha Sala, tawanyikeni katika nchi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufanikiwa} [62:10];

Yaani utakapomaliza Swala basi uende kwenye kazi zako za kidunia madamu ni halali na utafute kwenye kazi hizo ikhilasi, ukitarajia radhi za Allah; kama Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alivyomwambia mmoja wa sahaba zake:



### Akili na Mantiki

"Katika vivutio vya Uislamu ni kuwa kwake dini inayosimama kwa kutumia akili. Haumtaki kamwe mfuasi wake kufuta kipaji hiki alichopewa na Mungu. Kama ambavyo Uislamu unapenda utafiti na kuulizia mambo. Kadhalika inalingania wafuasi wake katika kusoma na kufanya utafiti, uchunguzi na kuangalia kabla ya imani. Uislamu unaunga mkono hekima isemayo: Thibitisha ukweli wa kila jambo kisha shikamana na kheri. Hili si jambo geni: Kwani hekima ni jambo lililompotea muumini popote alipatapo basi ni mwenye haki nayo zaidi. Uislamu ni dini ya matumizi ya akili na mantiki: Hivyo basi tunakuta kuwa neno la kwanza lililoshuka kwa Nabii Muhammad ni: "Soma", kama ambavyo tunaiona kauli mbiu ya Uislamu ni kulingania katika kuangalia na kutafakari kabla ya kuamini: Kwani Uislamu ni haki na silaha yake ni elimu, na adui yake mkubwa ni ujinga."

**Profesa Haroon Mustapha Lion**

Mwanazuoni wa Mambo ya Lugha huko Uingereza.

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

«Na wewe hutotoa matumizi yoyote ukitarajia nayo radhi za Allah isipokuwa utalipwa ujira hata kile ambacho utakiingiza katika mdomo wa mke wako.» (Imepokewa na Malik); Yaani katika mdomo wa mke wako unapata ujira, katika dini yetu hakuna kutenganisha kati ya dunia na akhera lakini kwa sharti ya kutoshughulishwa na dunia na kuacha akhera, kama alivyosema Allah Aliyetukuka:

{Enyi mlio amini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndio walio khasiri} [63:9]

Na akasema vile vile: {Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe….} [28:77],


Hivyo basi mapenzi ya matendo, mapenzi ya mke, kucheza na watoto na kuwajali, na mengine katika mipaka ya kisheria katika dini ni miongoni mwa uongofu wa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) iwapo kutakusudiwa radhi za Allah, Allah amesema: {Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.} [6:162],

## Suluhisho la Kiakili

"Qur-aan imeleta suluhisho la kiakili la matatizo ya zama hizi za Kiuchumi, kijamii na kimaadili: Kwa hili haiwezikani kutia shaka katika ile hekima ya Qur-aan kwa kuangalia mafanikio ya Muhammad katika kufikisha ujumbe ambao Mungu amemuarisha kuufikisha. Hivyo yapasa kwetu (kwa mtazamo wangu) kadiri ya misimamo yetu ya dini ilivyo kuzingatia ujumbe wa Qur-aan tangu kuchimbuka kwake huko Makkah."

**W. Montgomery Watt**

Mustashrik wa Kiingereza



Kwa hiyo maisha yote ni kwa ajili ya Allah, hata kile ambacho ndani yake kuna hadhi ya nafsi basi hicho ni kwa ajili ya kumtii Allah Aliyetakasika na kutukuka madamu nia imenyooka.

Amani ya nje pamoja na watu wa karibu na wa mbali, mwenye kuafikiana nae na mwenye kutofautiana nae, bali salamu ya kwanza anayomsalimia mtu nduguye ni kauli yake kwa nduguye; Amani juu yenu na rehema za Allah na baraka zake, watu hawakufurahi na kuhifadhika kwenye dini zote kama walivyofurahi katika utawala wa Uislamu; ni kiasi gani ulimwengu ulivyopata hasara kwa kuanguka kwa baadhi yaWaislamu, Allah amesema: {…Wala kuwachukia watu kwa kuwa wali-kuzuilieni kufika Msikiti mtakatifu kusikupelekeeni kuwafanyia uadui. Na saidianeni katika wema na uchamngu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu..} [5:2].



**Maisha Mazuri**

"Ikiwa tunataka kuwa waadilifu kuhusu Uislamu ni juu yetu kukubali kuwa katika mafundisho yake kunapatikana nguvu hii ambayo inawezekana ikawa maisha mazuri na haswa katika upande wa kimaadili. Mafundisho haya yanatakia rehema kwa viumbe vyote vya Mungu, na uaminifu katika mahusiano ya watu wenyewe kwa wenyewe, kadhalika mapenzi na ikhlasi na kuzuia silika zenye kuipelekea kwenye matamanio kama ambayo inavyowatakia mambo mengine mazuri.

Matokeo ya mambo yote haya ni kuwa Muislamu mwema anaishi maisha yenye uzalishaji mwingi kwa kadiri maadili yanavyohitajia."

**Ignaz Goldziher**

Mustashrik wa Kiyahudi.

## 7. Ustaarabu waUsawa na Mapenzi:

Ustaarabu wa Kiislamu unawajibisha Waislamu kuwa watu wenye nyoyo zilizosalimika na nafsi zilizo safi, amesema Allah Aliyetukuka kuhusu kisa cha dua ya Waumini: {Na walio kuja baada yao wanasema: Mola wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa Imani, wala usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walio amini. Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye kurehemu.} [59:10]



**Maadili ya Watu**

"Kwa hakika Waislamu kama wanavyojulikana ni watu waliokamilika zaidi kuliko Wakristo: Walikuwa ni watu wenye kulinda ahadi zaidi, wenye kuwahurumia zaidi wanaowashinda. Na makosa machache sana waliyofanya katika historia yao kuliko unyama waliofanya Wakristo walipotawala Qudsi mwaka 1099.

**Will Durant**

Mwandishi wa Kimarekani.

Na, {Siku ambayo kwamba mali hayato faa kitu wala wana. Isipo kuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo safi.} [26:88-89],

Na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema: «Msibughudhiane wala msihusudiane na kuweni waja wa Allah ni ndugu, haiwi halali Muislamu kumuhama nduguye zaidi ya siku tatu, hukutana huyu akampa mgongo huyu na mbora wao ni yule anayeanza kutoa salamu.» (Imepokewa na Muslim).


Na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema huku akihimiza mapenzi na kuzoeana: «Naapa kwa ambae nafsi yangu ipo mikononi mwake, hamtoingia peponi hadi muamini, na hamtoamini hadi mpendane, Je, nikujulisheni kitakachothibitisha hilo kwa ajili yenu? Enezeni salamu.» (Imepokewa na Tirmidhi).

Wakati fulani Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) aliulizwa: ni mtu yupi bora? Akasema: Kila mwenye moyo Makhmum, mkweli wa ulimi, wakasema: Mkweli wa ulimi tunamjua, basi ni nani Makhmumul-Qalbi? Akasema: «Huyo ni mcha-Mungu msafi, hakuna dhambi, wala uovu, wala kuvuka mipaka, wala husuda.» (Imepokewa na Ibn Majah).

## 8. Ustaarabu wa Kiroho na wa Kimada:

Ustaarabu wa Kiislamu umekuja kung'arisha roho za watu, na wakati huo huo haujasahau mada wala kuipuuuza, Allah amemuumba mwanadamu katika mada na roho, na kumpa sababu zote za maisha katika pande zake za kimada na kiroho; akatayarishia mwili mazingira yenye kufaa kuishi nayo katika uso wa ardhi, kadhalika Allah Aliyetukuka akaitayarishia chakula cha roho kutokana na wahyi wa mbinguni ambao Allah amemteremshia mwanadamu kupitia Mitume yake, Allah Aliyetukuka amesema: {Na Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Hakika Mimi nitamuumba mtu kwa udongo unao toa sauti, unao tokana na matope yaliyo tiwa sura. Basi nitakapo mkamilisha na nikampulizia roho yangu, basi mumwangukie kumsujudia.} [15:28-29],


**Dale Carnegie**
Mwandishi wa Kimarekani



## Starehe ya Kiroho.

“Kinachonishughulisha mimi sasa hivi ni ninachokipata katika neema za dini. Kama vile ambavyo ninajali neema tunayopata kutokana na umeme, chakula bora na maji safi. Haya yote hutusaidia kuishi maisha mazuri yenye neema. Ama dini hunipa mengi zaidi ya haya. Hunipa raha starehe ya kiroho, au hunipa (kama aliyozungumza William James) msukumo wa nguvu wenye kuunganisha maisha. Maisha yenye nafasi, yenye furaha maridhawa, kwa hakika inanipa imani, matarajio na ujasiri na huniondolea khofu, sononeko na wasiwasi. Vile vile hunielekeza kwenye malengo katika maisha na hukunjua mbele yangu upeo wa furaha na kunisaidia katika kujenga chemchem ya maji na rutuba katikati ya jangwa la maisha yetu.”

**Nassry Salhab**
Mwanafasihi wa Kilebanoni



## Ukubwa wa Uislamu

“Uislamu hauhitaji kalamu zetu kwa ufasaha wowote ule kalamu zetu zitakaoufikia. Lakini kalamu zetu zinauhitajia Uislamu, kwa yale ambayo Uislamu unayo kama vile utajiri wa kiroho na kimaadili kutoka kwenye Qur-aan yake nzuri ambayo kwake tunaweza kujifunza mengi.”

Hivyo basi roho na kiwiliwili ni vitu viwili vyenye kulazimiana kimoja hakitoki kwa mwenzake ila kwa mauti ya mtu.

Roho na kiwiliwili kila kimoja kina mahitaji na matakwa yake; kiwiliwili kinaishi kwa kula, kunywa na kuvaa hata kama kutakuwa na mapungufu upande mmoja utaona athari ya upande mwingine, kama mtu atakuwa amefanya mapungufu katika chakula chake utamkuta kuwa ni dhaifu anayeangamia hawezi kuishi maisha yenye utulivu na mazuri, vivyo hivyo kwenye kunywa na kuvaa.

Kwa hakika upungufu wa matakwa yoyote katika kiwiliwili hiki kinaakisi yote katika maisha yake, hawezi kuishi vizuri wala kusaidia upande wake wa pili (kiroho) katika maisha ya utulivu.

Hali kadhalika roho ina matakwa yake, roho haiishi bila mapenzi kutoa, wala kujitolea basi vipi roho itaishi bila mola inayemuabudu, kumpenda, kumtarajia, kumuogopa na kumkimbilia? Vipi roho itaishi ikiwa kifua kitupu haipati inayomtegemea na kutulia kwake, au haipati amani, kutoa na kusalimika moyo na mahaba baina ya watu?!

Ama kwa hakika mwanadamu akifanya mapungufu katika kuipa roho haja zake basi yeye ni kama aliyefanya mapungufu katika chakula chake na kinywaji chake, mwanadamu atatulia vipi, vipi hali yake itakuwa na utulivu na nusu yake ya pili hulalama na jeraha?! Kwa bahati mbaya ustaarabu wa Kimagharibi umesahau furaha ya roho na ndio maana ikawa na huzuni katika maisha haya ya dunia wakati ambapo yeye yupo katika kilele cha maisha mazuri, Ustaarabu wa kisasa ni ustaarabu uliopambazuka kwa kuhudumia kiwiliwili na Mada lakini umesahau au kujisahaulisha kiwiliwili bila ya roho ambayo haina furaha wala mafanikio wala utulivu, bali sio ustaarabu wa kweli.

## 9. Ustaarabu unaomjali mwanadamu na haki zake:

Limekuwa ni jambo maarufu kuwa utekelezaji wa haki za mwanadamu kuhesabiwa kuwa ni kigezo cha kujua kiasi ambacho nchi husika inazingatia misingi ya uadilifu, usawa, kulinda haki za wananchi wake na uhuru wao.

Kama ambavyo huzingatiwa kuwa ni kipimo cha ufahamu na mwamko wa wananchi kuneemeka na haki na uhuru wao, bali ni kipengele muhimu sana katika mifumo ya Kidemokrasia ambayo ni kulinda haki za wanadamu.

Katika Ustaarabu wa Kiislamu imejaa mifano mingi na ya kipekee katika uhalisia kuhusu haki za binadamu, nayo ndio ukubwa na utukufu wa ustaarabu huu wa Kiislamu, na kuwa sio maneno matupu tu au alama au kauli mbiu tu.

Mambo yenye kupambanua haki za binadamu katika Uislamu ni haya yafuatayo:

1. Chanzo cha haki hizi zimejengwa katika msingi kuwa ubwana na utawala ni wa Allah Aliyetukuka, Allah Ta'ala amesema: {…Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu. Yeye anasimulia yaliyo kweli; naye ni Mbora wa kuhukumu kuliko wote.} [6:57].

Hivyo basi sheria ya Kiislamu kuhusu haki huangaliwa kwa mtazamo wa kiiungu kwa kiumbe huyu, na yale yenye kumfaa.



### Aibu ipo Ndani Yetu

"Yapasa kuwa wazi kwetu kuwa Waislamu kupuuzia mambo (na sio upungufu katika mafundisho ya Uislamu) Hiyo ndio ambalo limesababisha matatizo tuliyonayo leo hii."

**Leopold Weiss**

Mwanafikra wa Austria.

2. Kuthibiti: Haibadiliki kwa kubadilika wakati na kubadilika mazingira na hali.


3. Kuchunga haki kulingana na msimamo wa hisani: Haki katika Uislamu zinaibuka kutokana na kisimamo ambacho ndani yake mja anakuwa chini ya kumuogopa Allah (Subhaanahu wa Ta'ala), nacho ni kisimamo cha hisani (wema) ambacho Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ameielezea: «Kumuabudu Allah kana kwamba unamuona, na kama humuoni yeye anakuona.» (Muslim).

4. Kuchanganyika na ukamilifu kati ya haki za binadamu na tabia ya dini hii:

Kwa hiyo Uislamu haukuacha haki hivi hivi tu, bali imezitengenezea mazingira ya hukumu za kisheria na katika mtazamo wa makusudio ya kisheria, na ikazilinganisha na adabu na maadili yake, na ikafanya kuharibu adabu zile ni kuharibu haki hizi, na mwishowe ni kuziunganisha na dini, na kuzingatia vyanzo vyake vya kiungu, na hivyo basi huhesabiwa kuwa ni majukumu ya Muislamu binafsi, na sio haki hivi hivi tu, hivyo basi kujenga haki katika Uislamu ni kujenga kwa ukamilifu wenye kulandana na tabia ya kiungu ya dini hii.



https://www.path-2-happiness.com/sw



## Amani ya Ulimwengu.

“Taarifa ya Qur-aan kuhusu Muumba wa Ulimwengu ilinitingisha: Nimeufahamu Uislamu kupitia Qur-aan, na sio katika matendo ya Waislamu. Enyi Waislamu kuweni Waislamu wa kweli ili Uislamu uweze kuenea ulimwengu. Kwani huo ni amani kwa ulimwengu wote.”

Cat Stevens.

Mwimbaji wa Uingereza.

5. Utawala wa mtu binafsi katika jamii ya kiislamu ndio msingi wa haki za binadamu katika Uislamu, na sio kinyume chake kama hali ilivyo katika sheria za wanadamu, Allah Aliyetukuka amesema:

{Kwa sababu ya hayo tuliwaandikia Wana wa Israili ya kwamba aliye muuwa mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote. Na hakika waliwajia Mitume wetu na hoja zilizo wazi. Kisha wengi katika wao baada ya haya wakawa waharibifu katika nchi.} [5:32].

6. Uislamu kutangulia katika haki za binadamu kabla ya wengine.

Kwa hiyo haki hizi ambazo Uislamu umedhamini kwa mwanadamu hazikuja katika mapambano ya kifikra au ya kimapinduzi na matakwa yake kama ilivyo katika historia ya haki za binadamu katika mfumo wa kidemokrasia na sababu za kuanza kwake, kama vile ilivyokuwa hali ya Ufaransa na Marekani na kwingineko, bali (haki hizi ambazo Uislamu umezidhamini) misingi yake imetulia na hukumu zake kwa Wahyi kutoka kwa Allah Aliyetukuka bila kuwepo mazungumzo yake kabla ya hapo au kuyafuatilia au mapambano ya kufikia njia yake.

7. Kuwa inafuata hali halisi na inaungana na maisha, hugusa haja ya mwanadamu; kinyume na haki katika sheria za kigeni –ambazo zimewekwa na kupambwa katika hali ya kifalsafa zaidi.

8. Kuna sheria ambazo ni za Uislamu peke yake, miongoni mwa haki hizo muhimu ni: haki za wazazi wawili, haki za ndugu kwa watoto, haki za jamaa wenye ndugu, haki ya kichanga tumboni, haki ya mtu kupata malezi ya kidini na ya kidunia, haki ya chumo halali, makatazo ya riba, haki ya kulingania katika kheri, kuamrisha mema na kukataza maovu.

9. Suluhisho la Uislamu kuhusu kadhia za haki za binadamu inasimama katika asili ya utu wa mwanadamu na kuchochea hisia ya imani kwa Allah Aliyetukuka, kinyume na sheria zingine. Haki hizi zinaegemea katika ufahamu wa kuwa ulimwengu huu umedhalilishwa na Allah Aliyetukuka kwa maslahi ya binadamu kulingana na kanuni za kimaumbile. Historia ya mwanadamu haikuwa kushuhudia ustaarabu ambao umetekeleza haki za mwanadamu pasipo maslahi (ya watawala), vinginevyo tunaona kwa wepesi nembo zinazotolewa na wito mwingi na kunyanyuliwa kwa mabango, lakini ni ugumu ulioje kugundua hakika zilizojificha nyuma yake na nia zilizo funikwa nyuma yake pindi wale viongozi wake wanapokuwa chini ya viwango vya utata….

https://www.path-2-happiness.com/sw



Pamoja na ustaarabu huu kuwaenea wanadamu kwa kutumwa kwake, ila ni kuwa baadhi ya watu wanaweza kujiuliza-kuhusu sababu za kurudi nyuma Waislamu na kuwa kwao katika hali waliyonayo leo hii pamoja na maendeleo haya ya Ustaarabu wa Kiislamu?!

Hata hivyo kushangazwa huku kunaondoka tukifahamu hali ya Waislamu leo hii haiwakilishi ukweli wa dini yao, wengi wao wamerudi nyuma pindi walipoacha misingi ya dini yao na yaliyokuja kwenye kitabu chao na katika Sunnah ya Mtume wao (Swala Llahu 'alayhi wasallam), vinginevyo dunia isingefahamu ustaarabu uliofurahisha walimwengu wote kuliko ustaarabu wa Kiislamu, inatosha kusoma historia na kusikiliza kauli za waadilifu hata wasiokuwa Waislamu ili tuone ni kwanini ulimwengu umepata hasara kwa kuparaganyika Waislamu?!



## Ulimwengu Mtupu

"Inawezekana Waislamu wakasambaza ustaarabu wao katika ulimwengu kwa haraka ile ile ambayo walioisambaza hapo kabla: Kwani ulimwengu huu mtupu hauwezi kuthubutu mbele ya Roho ya Ustaarabu wao."


**Marmaduke Pickthal**
Mwandishi wa Uingereza

https://www.path-2-happiness.com/sw



# MIUJIZA KATIKA QUR-AAN NA SUNNAH

Kila Mtume ana miujiza inayothibitisha ukweli wa utume wake na ujumbe wake, kwa mfano miujiza ya Musa ('Alayhi Salaam) ilikuwa ni ile fimbo yake, na miujiza ya Issa ('Alayhi Salaam) ilikuwa ni kuponya mbalanga na ukoma na kuhuisha mauti kwa idhini ya Allah. Ama miujiza ya Mtume wa mwisho inawiana kwa kila zama na mahali muda wote mwanadamu akiwepo na ndio hii Qur-aan Tukufu, na ikiwa Qur-aan Tukufu ni kitabu cha mwongozo; basi kitabu hiki kitukufu ni miujiza wa kila kitu, na miujiza yake ni kusadikisha ukweli na utume wa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kuwa yeye ametumwa na Muumba, mwenye kutoa riziki Msimamia mambo yote milele, na kuwa ni kitabu alichotumwa nacho mwisho wa Mitume na Manabii, inayofaa kila zama na mahali na sehemu zake za miujiza yake ambazo tumezitaja huko nyuma; kwa hakika Qur-aan ni muujiza wa kisayansi na elimu mbali mbali kama ilivyokwisha oneshwa na watafiti wa kisasa katika kubainisha kuwa Qur-aan kugusa kwake mambo ya ndani ya kisayansi ambayo hayakuvumbuliwa isipokuwa katika karne hii, miongoni mwa hayo kwa mfano: awamu za kuumbwa mwanadamu na kitoto kilicho tumboni katika wasifu makini kabisa na wa ndani kabla watu hawajaweza kulijua hilo kwa mamia ya miaka, Allah Aliyetukuka amesema: {Na kwa yakini tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo. Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti. Kisha tukaiumba tone kuwa damu iliyo ganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama. Kisha tukamfanya kiumbe mwengine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji. } [23:12-14]



Na akasema Aliyetukuka: {Amekuumbeni kutokana na nafsi moja. Kisha akamfanya mwenziwe katika nafsi ile ile. Na akakuleteeni wanyama wa mifugo jozi nane. Anakuumbeni katika matumbo ya mama zenu, umbo baada ya umbo, katika viza vitatu. Huyu ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi. Ufalme ni wake. Hapana mungu isipo kuwa Yeye. Basi nyinyi mnageuzwa wapi?} [39:6]

Na pindi madaktari waliporejea katika rejea zao na katika ugunduzi wao walipata kama alivyosema Mjuzi wa yote.

Kwa kuongezea kubainisha sehemu ya hisia ndani ya mwili, Allah amesema: {Hakika wale walio zikataa Ishara zetu tutawaingiza Motoni. Kila zitapo wiva ngozi zao tutawabadilishia ngozi nyengine ili waionje hiyo adhabu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.} [4:56],

Na ubainifu wa upana wa anga, Allah Aliyetukuka amesema: {Na mbingu tumezifanya kwa nguvu na uwezo na hakika Sisi bila ya shaka ndio twenye uwezo wa kuzitanua.} [51:47],

Na kubainisha mzunguko wa jua katika mzunguko wake, Allah Aliyetukuka amesema: {Na usiku ni Ishara kwao. Tunauvua humo mchana, mara wao wanakuwa gizani. Na jua linakwenda kwa kiwango chake. Hayo ni makadirio ya Mwenye nguvu, Mwenye kujua. } [36:37-38].



## Wasifu wa Kichanga

"Sipati tabu kukubali kuwa Qur-aan ni maneno ya Mwenyezi Mungu, kwani wasifu wa kichanga kilicho tumboni katika Qur-aan hauwezi kujengwa juu ya utaalamu wa kisayansi wa karne ya saba. Matokeo pekee yanayoweza kukubalika ni kuwa wasifu huu ni WAHYI (UFUNUO) alioupata Muhammad kutoka kwa Mungu."

**Profesa Yushudi Kusan**

Mkuu wa Kituo cha Anga Tokyo.

Hali kadhalika Sunnah Tukufu ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) haikujitenga na miujiza hiyo; kutoka kwa Ummul Muuminina bibi Aisha (Radhiya Llahu 'anha) amesema: amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam); «Hakika kila mwanadamu ameumbwa kutokana na mwanadamu kwa viungo mia tatu na sitini, yule atakayesema takbira, atakayemhimidi Allah, na akasema: 'La illaha illa llah, akamsabihi Allah, akamuomba msamaha, na akaondoa jiwe kwenye njia za watu, au mwiba, au mfupa au kuamrisha mema au kukataza maovu akahesabu miaka ile miaka mia tatu na sitini mifupa na viungo vya mwili basi mtu huyo hufika jioni akiwa ameepushwa na moto.» (Muslim).

Kilichothibiti kisayansi leo hii ni kuwa bila ya viungo hivi katika mwili wa mwanadamu, asingeweza kuwepo katika maisha haya, wala kusimamia majukumu yake ya ukhalifa ardhini, na ndio maana inapasa mwanadamu kushukuru Allah Aliyetukuka kila siku kwa neema hii ambayo inathibitisha uwezo wa Muumba juu ya kila kitu.

Jambo la muujiza katika Hadithi hii ni kuainisha kuwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) idadi ya viungo vya kiwiliwili cha mwanadamu ni ainisho la kina kabisa katika zama ambazo hakukuwepo elimu hiyo kwa yeyote aliyeumbwa.

Watu wengi leo hii katika karne hii ya Ishirini na moja hawajui hilo, bali hata baadhi ya walimu wa tiba hawafahamu hilo!!! Hadi walipovumbua hivi karibuni kuwa idadi ya viungo vya mwanadamu ni mia tatu sitini kama ilivyoainishwa na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kabla ya karne kumi na nne zilizopita ambazo ndani ya viungo hivyo, viungo mia moja arubaini na saba (147) vya uti wa mgongo na Ishirini na nne (24) viungo vya kifuani na themanini na sita (86) ni viungo vya nusu ya juu ya kiwiliwili na themanini na nane (88) ni viungo vya nusu ya chini, na kumi na tano (15) na viungo vya Hodhi.

Swali linalojitokeza hapa: Kama sio Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) Muumba Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) angewezaje kujua hakika hii ya kisayansi ya ndani zaidi, ambayo elimu ya mwanadamu haijaweza kuifikia ila mwishoni mwa karne ya Ishirini?!!

Nani ambaye anaweza kumlingania Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kuzamia mambo ya ghaib kama haya?! Kama sio Allah Aliyetukuka anayejua kwa elimu yake iliyozunguka kila kitu kuwa mwanadamu atafikia siku moja kufahamu hakika hii ya kielimu ya

upasuaji kiwiliwili cha mwanadamu, na hivyo hili kuwa ni mng'ao wa nuru katika hadithi hii tukufu kuwa ni uthibitisho wa utume wa Mtume huyu wa mwisho kwa ukweli wa muungano wake na Wahyi wa mbinguni.

Hata hivyo njia ya elimu na ustaarabu madamu kama haitakuwa ni njia ya maadili basi ustaarabu huo utakuwa ni wenye kuangamiza na elimu yake itakuwa ya maangamizi na sio ya kuwafurahisha watu na kuwahudumia! Vivyo hivyo njia ya elimu na ustaarabu vile vile ni njia ya maadili, kama ambavyo njia ya furaha bila ya elimu na ustaarabu ni upotofu, na hali kadhalika njia ya elimu na ustaarabu bila ya maadili ni yenye kuangamiza watu, Umma na jamii za wanadamu.





**Mtume Umiyi (Asiyesoma Yaliyoandikwa).**

"Akili inashangaa! Iweje ayah zile zitoke kutoka kwa mtu asiyeweza kusoma yaliyoandikwa. Watu wote wa Mashariki wamekubali kuwa ni ayah ambazo fikra ya mwanadamu haiwezi kuleta mfano wake kwa lafudhi na maana."

**Henri de Castriesry**

Luteni wa Jeshi la Ufaransa

**Miujiza ya Ulimwengu.**

"Vipi aliweza Muhammad, mtu asiyesoma yaliyoandikwa, aliyeishi maisha zama za Ujinga aweze kujua miujiza ya Ulimwengu iliyoelezwa kwenye Qur-aan Tukufu, ambazo sayansi leo hii bado zinaendelea kushughulikia?! Bila shaka hapana budi basi maneno haya kuwa ni maneno ya Mwenyezi Mungu."

**Deborah Potter**

Mwanahabari wa Kimarekani.

